



MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA (TANTRADE)

MHUTASARI WA MAFUNZO YALIYOTOLEWA KWA WASINDIKAJI WA MCHELE NA WAFANYABIASHA (SMEs) 250 WALIOJENGWEA UWEZO WA KUHUDUMIA MASOKO YA NDANI NA NJE, KATI YA FEBRUARI HADI JULAI, 2021.

HALI YA SEKTA NAFKA YA MCHELE

Mchele ni miongoni mwa mazao ambayo hunazalishwa kwa wingi nchini baada ya Mazao ya mahindi. Uzalishaji wa mpunga unakadiriwa kuwa takribani tani milioni tano na laki mbili (5.2) ambapo unapelekea kupatikana kwa mchele usiopungua kiasi cha tani milioni Mbili (2,2). Kipindi cha Mwaka 2020/2021 kumekuwa na ongezeko la uzalishaji ikilinganishwa na mahitaji na hivyo kuonesha uhitaji wa kuboresha zaidi sekta hiyo kibiashara ili mazao yakidhi ushindani wa Masoko ya Ndani na Nje.

MAELEZO YA PROGRAM

- Kutokana na umuhimu wa Sekta ya mchele na mchango wake kwenye Lishe, Ajira, Kipato na ukuaji wa Viwanda, TanTrade ilishirikiana na Taasisi ya Baraza la Mchele Tanzania (RCT) chini ya ufadhili wa Taasisi ya Kuendeleza uzalishaji endelevu wa mchele (Rikolto) na Wadau wengine, kuendesha semina kwa Wazalishaji wa Mpunga na Mchele ili kuwawezesha kuboresha mazao yao na kuwa na mikakati endelevu ya kuyafikia Masoko. Wadau muhimu walionufaika na mafunzo ni pamoja na Wazalishaji wa Mchele wa Magugu chini ya Skimu mbalimbali Wilayani Babati Mkoani Manyara Tarehe 25.05.2021 na Wazalishaji wa Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha mnamo tarehe 27.05.2021.
- Mafunzo kama hayo yamefanyika pia kwa wazalishaji na Viongozi wa Skimu za maeneo ya Kivulini, Kileo na Kirya katika Wilaya ya Mwanga Mkoani Kilimanjaro, mnamo tarehe 28.05.2021

- Mpango huu ulikuwa ni muendelezo wa Mafunzo na huduma za ushauri ambao ulifanyika awali kwa Wadau wa Nafaka katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika maeneo ya Mbarali Mkoani Mbeya, Ruaha Mkoani Iringa na pia Kilombero, Ifakara na Malinyi kwa Mkoa wa Morogoro na baadae Kahama Mkoani Shinyanga katika kipindi cha *Februari hadi Mei 2021* ambapo wazalishaji na Wasindikaji (SMEs) zaidi ya 250 walinufaika katika maeneo yaliyotajwa.

(Picha: Wadau wa mpunga skimu za Arumeru wakipatiwa elimu ya uzalishaji wenye tija 25.05.2021)



MAFUNZO YALIYOTOLEWA

- Wadau wameshauriwa mambo yafuatayo:-
- Namna ya kuongeza uzalishaji kwa matumizi ya mbegu bora na Viwatilifu kwa muda sahihi;
- Uvunaji, ukaushaji na uhifadhi mzuri wa mpunga ikiwa ni pamoja na uchakataji wenye kuzingatia viwango ili kuweza kupata mchele mzuri;
- Wasindikaji walielimishwa kuhusu mbinu bora za ufungashaji wenye kuzingatia ujazo, uwekaji wa chapa na rajamu (Branding) kama sehemu ya mkakati wa kufanikisha masoko;
- kufuatilia taarifa za mwenendo wa masoko ya mchele ili kuwawezesha
- Wazaliashaji kujipanga na kuzingatia mahitaji ya masoko;
- na pia kuimarisha vyama vyao vya ushirika ili kupunguza gharama zinazolazimisha kuuza mchele wao bei ya juu kuliko uhalisia wa Masoko.

(Picha: Mfano wa chapa/mchele ulioongezwa thamani na kufungashwa vizuri kwa ajili ya Masoko ya ndani na nje)



USHAURI MUHIMU ULITOLEWA

Wazaliashaji wameshauriwa kuongeza kiasi cha uzalishaji na ubora kwa kuzingatia aina za mbegu na kuweka mchele wao katika madaraja mbalimbali ili kuweza kufikia masoko Makubwa. Vilevile Wadau wamehamasishwa kushughulikia ufungashaji na utiaji wa Rajamu/Chapa ili mchele uweze kuwa na Taswira nzuri yaani 'Brand' kwa walaji tofauti na hali ilivyo hivi sasa wengi wanauza mchele wao katika magunia yasiyo na vipimo vya uhakika. Pia wazaliashaji wameshauriwa kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na TanTrade ili kupata hali halisi ya soko ili wazalishe kwa faida.

(Picha: Baadhi ya chapa za SMEs- wanufaika wa huduma za mafunzo na ushauri katika uongezaji thamani na Masoko zilizofanyika kati ya Februari na June 2021)



MATOKEO YA USHAURI NA MAFUNZO:

- Baada ya program za ushauri kutolewa Makampuni kadhaa (SMEs) ikiwemo Ruaha na Kibu-Agribusiness Limited tayari yameanza mauzo nchini Kenya, Uganda na Rwanda na hivyo kuwa na fursa kuweza kuhudumia zaidi ya tani 250 za mchele kwa mwezi, nchini Kenya zenye thamani ya takribani milioni 400
- Wadau wanaendelea kushauriwa na kuunganishwa na fursa za Masoko yanayopatikana.

- ✓ Je unahitaji Mafunzo katika Ujasiriamali na uendeshaji Biashara?
- ✓ Unahitaji mafunzo na ushauri kuhusu taratibu na nyaraka za mauzo Nje?

KARIBU!

❖ Kufahamu namna unavyoweza kupata huduma za TanTrade/Kitengo cha SMEs Tembelea ofisi za TanTrade au tuandikie ujumbe wa Barua pepe: info@tantrade.go.tz